# Vibarua walia na madalali wa soko la Mwanza

## ■Wadaiwa kufaidika kwa migongo yao

NA ANGELA SEBASTIAN

UMASIKINI wa kipato ni tatizo linalowakumba watu wengi nchini.

Hii inatokana na hali duni ya maisha, watu kulipwa ujira mdogo katika maeneo wanayofanyia kazi, lakini dhana nzima inabaki katika suala la hali ngumu ya uchumi.

Kutokana na ukweli huo,kila mtu katika eneo analofanya kazi, angependa alipwe vizuri ili kukabiliana na changamoto za maisha.

Hilipaji vizuri unaweza kufanywa katika maeneo ambayo ajira zinafanywa kwa kufuata sheria za nchi.

Lakini kuna baadhi ya maeneo hasa katika sekta zisizo rasmi, wafanyakazi hasa vibarua wamekuwa wakinyanyaswa kwa kulipwa ujira mdogo licha ya kazi ngumu wanazofanya.

Hawa hujikuta wakishindwa mahali pa kupeleka malalamiko yao kutokana na kukosa chombo kinachowatetea au kusimamia maslahi yao.

Baadhi ya watu hao ni wale vibarua hasa wanaofanya kazi katika masoko kama vile wale wanaoshindilia dagaa katika soko kuu la Mwaloni, jijini Mwanza.

Licha ya kazi ngumu na vumbi lukuki inayoweza kuathiri afya zao, wafanyakazi hawa hulipwa ujira wa sh. 10,000 kwa siku baada ya kushindilia magunia 40.

Akizungumza na waandishi wa habari, Anitha Sosthenes (26) anayefanya kazi ya kupakia dagaa katika magunia alisema kazi hiyo ni ngumu na inahitaji uvumilivu wa hali ya juu.

"Tunalipwa kiasi kidogo sana cha fedha hivyo kushindwa kumudu gharama za maisha, lakini binafsi inabidi nifanye kazi hii kwani sina pa kwenda," alisema.

Anasema kutokana na kupanda kwa maisha hata mtu asiye na familia hawezi kutosheka na kiasi hicho.

"Kwakweli kila kazi ina uzuri wake na changamoto zake hata hivyo hii ya kwetu imezidi, ni ngumu kama unavyoona, vumbi nalo linatuathiri, malipo ndiyo hayo, fikiria upakie magunia 40 kwa siku malipo ni shilingi elfu kumi kwakweli na hali ya uchumi ya sasa kiasi hicho kinatanisadia nini?" alihoji.

Analalamika kuwa ujira huo kwa siku inabidi wautumie pia kwa kununulia chakula asubuhi na mchana pamoja na jioni, lakini kutokana na pesa kuwa ndogo, hulazimika kula mlo mmoja kwa siku ili kujiwekea akiba.


Mwanamama huyu anasema kutokana na matumizi ya kila siku, hujikuta akibakiwa na sh. 1,500.

Hata hivyo, wafanyabiashara wanaonunua dagaa hao wanadai kuwa madalali ndiyo wanaohusika kuwapunja vibarua wao.

John Ng'ala mfanyabiashara kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anasema utaratibu wanaofanya ni kuchukua mzigo kwa madalali na hawahusiki na vibarua hao.

"Sisi tukifika tunachukua mzigo kwa madalali, hatujui mapatano yao," alisema.

Uzoefu unaonyesha kuwa, madalali huchukua mzigo kwa wanaovua dagaa na wafanyabiashara wadogo wao kuuza kwa



wafanyabiashara wakubwa.

Naye Mwenyekiti wa Soko hilo, Chri
Wankyo alieleza kuwa tatizo hilo lipo la
kubwa vibarua na wafanyabiashara hao
wakiwekeana mikataba kwa kificho.

Alisema kama vibarua wangetaka ku
wangeushirikisha uongozi na kuweka w
yao, ili walipwe anagalia ujira unaoelew

Wankyo alisema inakuwa vigumu ku
biashara hizo kutokana na kutoshirikish
moja.

"Wangekuwa wanatushirikisha kama
wakati wanapoandikiana mikataba wa k
kazi zao ingesaidia sana, wao hufanya k
kwa madai kuwa biashara ni siri matoke
kudhulumiwa kwa kulipwa ujira mdogo,"

Alisema kuna baadhi ya vibarua huny
pesa pindi wanaposhindwa kujaza magu
wanayoafikiana kwa siku.

"Unajua, Watanzania wengi hatuna st
ujasiriamali ambazo zinaweza kutufanya
na hii hali ya kutumikishwa katika ardhi
inasikitisha sana kuona mtu anatakiwa k
magunia 40 kwa ujira wa sh.10,000 nad
umefika wa kuondokana na hali hii ni ju
sote," alisema.

Akiwasilisha mada katika mafunzo ya
wa habari za biashara na uchumi, Dk. Od
alisema: "Ili taifa liendelee ni vema likaw
watu wake kwa kuhakikisha wana stadi a
zitawawezesha kusukuma maendeleo ya

Alisema ukosefu wa stadi hizi ndo una
watanzania wengi kujikuta wanakosa uza
hivyo kuwatumikisha wenzao kama watu

Bilame alisema ukosefu wa stadi pia u
Watanzania na hasa wa kipato cha chini k
kuendesha maisha yao na hivyo kujikuta
wakitumikishwa kwa kazi ngumu na kuli
mdogo.



> "Kwakweli kila kazi ina uzuri wake na changamoto zake hata hivyo hii ya kwetu imezidi, ni ugumu kama unavyoona, vumbi nalo linatuathiri, malipo ndiyo hayo, fikiria upakie magunia 40 kwa siku malipo ni shilingi elfu kumi kwakweli na hali ya uchumi ya sasa kiasi hicho kinatanisadia nini?"

# Wafanyabiashara wanapoponzwa na Kiswahili nchini Uganda



*MKULIMA akitoa ndizi shambani. Biashara hiyo imewasaidia wakulima kuondokana na umasikini.*

ANGELA SEBASTIAN

AMANI ni tunda la maendeleo. Kwa maana hiyo, taifa linalokabiliwa na vita na machafuko, maendeleo ya watu wake yanazidi kudidimia kwa watu kufa na miundombinu kuharibiwa.Kwa hiyo, fursa muhimu za kuwaendeleza watu zimekuwa zikipatikana katika jamii ambazo watu wake wana uhakika wa kujishughulisha kiuchumi bila kuwepo kwa bugudha.

Hiyo ni sawa na kueleza kwamba amani iliyopo Tanzania inanufaisha wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali duniani na matokeo yake, wakati mwingine kutumia fursa hiyo vibaya kwa kuwanyonya wazawa.

Pamoja na fursa hiyo adhimu, changamoto zingine zimekuwa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kupata misukosuko katika soko la Afrika Mashariki kutoka na utu wao.

Shukuru Mwesigwa ambaye ni mkulima, anaeleza kwamba aliwahi kupeleka ndizi nchini Uganda katika mlolongo wa kuimarisha soko la Afrika Mashariki lakini alikamatwa na kunyanyaswa.

"Nilipoona biashara ya ndizi inachanganya, niliamua kukopa fedha kiasi cha shilingi milioni moja kutoka NMB, nikakodi gari na kupakia mzigo nikiwa na vibali vyote, nikasafirisha mpaka Kampala na kuanza kutafuta wateja siku hiyo.

"Jambo la kushangaza, tuliposikika tukiongea Kiswahili na dreva wangu tuliambiwa tuwakopeshe mzigo, kwani wafanyabiasha wanaokwenda huko toka Tanzania huwakopesha halafu pesa baadaye," anasema na kuongeza.

"Tulikaa siku tatu mpaka ndizi zikaanza kuiva ndipo nikaamua kumkabidhi tajiri mmoja aitwaye Matovu na kuniahidi nirudi kesho yake mchana nikachukue pesa yangu," anaeleza.

Mwesigwa anasema kwamba alitegemea kupata zaidi ya sh.milioni 1.7 lakini akaambulia shilingi milioni moja ambayo hajapewa yote, zaidi ya kuambulia shilingi laki tano na baada ya kudai fedha iliyobaki, alipelekwa polisi kuwa yeye ni Mtanzania ana Kiswahili kirefu.

Pamoja na kupelekwa polisi, pia alidaiwa tapeli, hata hivyo wafanyabiashara wa Tanzania waliokuwa huko kibiashara walipata taarifa kukamatwa kwake ambapo walimwekea dhamana polisi alikokaa siku tatu na kuamriwa kulipa faini ya sh.300,000 na kujikuta akifilisika.

Ili kuhakikisha analipa mkopo benki, alilazimika kuuza pikipiki yake ambayo ilikuwa ikimuingizia kipato cha sh.42, 000 kwa wiki na kulipa deni hilo.

"Kumbe amani ya Tanzania inawanufaisha watu kutoka nje. Hata hii dhana ya soko la pamoja la Afrika Mashariki haiwezi kufanikiwa kwani wenzetu wanataka twende kwao tununue vitu vyao lakini hawataki tupeleke vitu vyetu, wanataka waje huku wanunue kwa bei wanayoitaka kwa kutupunja," anasema Mwesigwa.

Anasema kutokana na amani kuwa ndogo na ushirikiano mdogo uliokuwa nchini Uganda imewafanya kuwaachia Waganda waendelee kunufaika na uwepo wa soko hilo la ndizi na wao kuambulia kazi za upakiaji katika malori.

Martin Natukunda ambaye ni mfanyabiashara wa ndizi kutoka nchini Uganda anaeleza kuwa biashara ya ndizi inaendelea kuwapa faida, kwani wao wananunua kwa sh.3,000 mpaka 5,000 kwa mkungu wa ndizi na wao huuza kuanzia sh.8,000.

Anafafanua kuwa mikungu mikubwa ya ndizi hununua kwa sh.8,000 na kuuza mnadani kwao kwa bei ya sh.15.000 hadi 20.000, ambapo inadaiwa hupeleka Sudan ndizi hizo ambako kuna soko la uhakika

"Biashara hii imekuwa na mafanikio kwetu, ndiyo maana tunaona tunaendelea nayo mpaka leo," anaeleza.

Katika kujinasibu huko, anaeleza kuwa kutokana na mahitaji makubwa ya ndizi nchini Sudan imekuwa ikiwachukua siku tatu hadi sita kurudi tena mkoani Kagera kuchukua mzigo mwingine kwa ajili ya wateja wao.

Hata hivyo, anasema wafanyabiashara wa Kitanzania wameshindwa kupata fursa ya kupeleka ndizi na bidhaa nyingine Uganda na maeneo mengine ya nchi za Kiafrika kutokana na kuhofia usalama wao na mali zao na kuwa ushrikiano kwao kwa wafanyabiashara kutoka nje ya nchi ni mdogo.

"Amani, upendo na utulivu na mazingira ya kuridhisha ya ufanyaji biashara mbali na matatizo mengine yaliyoko Tanzania, kule kwetu ni kitendawili, kwa hiyo nawaomba Watanzania kudumisha hali hiyo ili kuongeza wateja, nao wawe wathubutu wa kuvuka mipaka kwenda Uganda na kwingineko ili wanufaike na soko la pamoja la Afrika Mashariki," anashauri Natukunda.

Mkulima Salome Mwijage kutoka Kijiji cha Mbatama, Bukoba Vijijini anaeleza kuwa changamoto hiyo inaweza kutatuliwa iwapo itafufua viwanda vya ndani kama vya kutengeneza kinywaji cha wine inayotokana na ndizi.

Kazi ambayo huifanya kutokana na mafunzo waliyonayo baadhi ya wakulima kutoka kwa wataalam wa Viwanda VidogoVidogo(SIDO) ni usindikaji, ambao hauwezi kuwasaidia kwa kuwa hawawezi kuuza nje ya eneo hilo na kwa gharama kubwa .

Kwa hali hiyo, kukifufuliwa viwanda hivyo kutasaidia taifa kupata mapato kuliko ilivyo sasa, pia watatengeneza ajira kwa Watanzania ambao mchango wao utaisaidia kuongeza mapato.

Kanali Mstaafu, Fabian Masawe, ambaye ni mkuu wa mkoa wa Kagera anasema kwa kipindi cha mwaka jana katika mpaka wa Tanzania na Uganda eneo la Mutukula kwa upande wa Tanzania, soko la ndizi lilikuwa kubwa.

Masawe anaeleza kuwa lengo lilikuwa kuondoa ulanguzi kwa zao hilo ili wakulima waweze kufika hapo na kuuza wenyewe na kunufaika na bei uzuri ya mazao yao huku serikali ikijipatia ushuru, ambapo kila gari liliweza kulipia kiasi kisichopungua sh.10,000 baada ya kupakia.

Anasema hayawahi kusikia mtu akilalamikia matatizo yanayowakumba Watanzania wakienda Uganda, kwani soko la ndizi liko upande wa Tanzania.

Kwa hiyo, kama kuna mtu kafanyiwa hivyo na hakutoa taarifa inawezekana akawa mmoja wa walanguzi wanaonunua kinyemela shambani kwa wakulima kwa kuwalaghai.

Anaeleza pia kuwa ameziagiza halmashauri zote za mkoa huo kupitia miradi ya kilimo kuwapa elimu ya ujasiriamali wakulima ili kujipatia ujuzi ambao utawasaidia kupeleka mazao yao kwenye soko bila kutegemea walanguzi■



# Elimu iliyopatikana Uganda itumike kutokomeza ugonjwa wa migomba

NA ANGELA SEBASTIAN

KUTOKANA na umuhimu wa kilimo kwa wananchi, serikali imekuwa ikifanya kila jitihada kuhakikisha wakulima wananufaika.

Ni kwa misingi hiyo, hivi karibuni serikali ilikubali kutoa sh. milioni 25 kwa lengo la kuwawezesha wakulima wapatao [illegible] kutoka Bukoba Vijijini kwenda Uganda kujifunza jinsi ya kudhibiti na kupamba na ugonjwa wa mnyauko wa migomba kutoka kwa wakulima wenzao wa vijiji vya Bukara [illegible] Rubagano, Ggwampala, Kigaga na Kabagaga.

Fedha hizo zilitolewa baada ya jitihada kubwa kufanywa na Mbunge wa Bukoba Vijijini, Jason Rweikiza.

Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Christopher Chiza [illegible] fedha hizo ziliombwa na mbunge huyo Februari mwaka huu baada ya kuona tatizo la ugonjwa huo linavyoathiri Bukoba Vijijini.

Lengo lilikuwa kuhakikisha wakulima waliokumbwa na tatizo hilo wanapata elimu kwa wenzao wa Uganda ambao wameweza kudhibiti ugonjwa huo na kuumaliza kabisa.

Chiza anasema, tayari fedha hizo zimetolewa na wakulima wamekwenda kujifunza mbinu za kupambana na kupambana na kutokomeza ugonjwa wa mnyauko wa migomba.

Mapema mwaka huu, Rweikiza alikwenda Uganda akiambatana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Anna Tibaijuka na mkuu wa Mkoa wa Kagera baada ya kupata mwaliko kutoka kwa Rais Yoweri Museveni kwa lengo la kujifunza kilimo bora na jinsi ya kuzuia magonjwa ya migomba.

Rweikiza anasema walipofika walitembelea mashamba ya wakulima mbalimbali ambapo walielezwa kwamba miaka mitatu iliyopita kulikuwa na ugonjwa wa mnyauko wa migomba ambao unakausha migomba kuanzia majani, shina mpaka mizizi, ugonjwa uliowasumbua sana, lakini sasa wameweza kuudhibiti na kubaki historia.

"Kusema ukweli ugonjwa huo umetuathiri sana Bukoba kwani ndizi ndio tegemeo letu kwa chakula na biashara. Waganda walitueleza mbinu nyingi walizotumia kwa hiyo pindi niliporudi niliamua kupeleka maombi serikalini ili kupata fedha za kuwapeleka walioathiriwa na ugonjwa huo ambapo vijiji 92 viliathirika na kusababisha [illegible] hilo kuanzishwa," anasema Rweikiza.

Anawashauri wakulima waliojifunza mbinu za kupambana na ugonjwa huo kuongeza jitihada ili kuutokomeza kabisa.

## WAKULIMA WA TANZANIA NA UGANDA WANAVYOSEMA

Respikius Mutagahywa ni mkulima wa ndizi kutoka Kata ya Kanyangereko Bukoba Vijijini anasema wamejifunza mambo mengi ila jambo la msingi ni jinsi wenzao wa Uganda walivyoweka nguvu ya pamoja kuondokana na kero ya ugonjwa wa mnyauko.

"Wenzetu wamekuwa wakitumia dawa aina ya jick kuoshea mapanga, majembe, viosho na vifaa vingine vinavyotumika katika mashamba yao ya migomba kwa kupalilia na kufyeka na wale wasiokuwa na uwezo wa kupata dawa hiyo wanashauriwa kufyeka shamba zima na kukusanya migomba hiyo na kuichomea sehemu moja na endapo watagundua ugonjwa huo hata kama ni mgomba mmoja kati ya migomba 100 ulioathirika unaondoa yote," anasema.

Respikius anasema hatua hiyo imewasaidia sana kuondoa kabisa ugonjwa huo tofauti na wakulima wa Bukoba ambao jitihada zao sio kubwa sana licha ya kuwa wamepewa mafunzo na watafiti.

Jakson Kabwisho (74) ambaye ni mkulima katika kijiji cha Rubagano wilaya ya Mbarara, Uganda anasema pamoja na njia mbalimbali wanazotumia, walihakikisha sheria ndogo ndogo zilizoko chini ya halmashauri zinatumika ipasavyo na kuwapa nguvu maofisa ugani kuhakikisha wanapita kila shamba na kukagua.

Anasema pindi akibainika mtu kagundua ugonjwa huo na kagoma kufuata sheria ya kufyeka migomba na kuichoma ili usienee kwingine anakamatwa na kutozwa faini au kifungo kisichopungua mwaka mmoja jela au vyote kwa pamoja, kwa hiyo hatua hiyo imewafanya wakulima kuitikia wito wa mapambano hayo hatimaye kuumaliza kabisa.

Mugenzi Byabachwezi ambaye ni mratibu wa mradi wa migomba mkoani Kagera kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Maruku (ARID) anasema ugonjwa huo kwa mara ya kwanza uliingia Uganda mwaka 2005 ambapo ulisambaa mpaka Tanzania katika vijiji vilivyoko mpakani. Anaongeza kuwa baadaye ulisambaa maeneo mengine.

Mtafiti wa kilimo Dk Jerome Kubiriba ambaye ni mtaalamu kutoka taasisi ya utafiti ya Uganda (National Agriculture Reserch Organasation) (NARO) anasema ugonjwa wa mnyauko wa migomba sio jukumu la kuwaachia wakulima pekee, kwani ni kazi kubwa inayohitaji ushirikiano na hamasa kati ya viongozi wa kisiasa na kijamii kwa ujumla.


Ana kuwa si jambo la busara kwa viongozi wa kuchaguliwa kukimbilia kuomba kura kutoka kwa wananchi wakati wa uchaguzi huku wakishindwa kuonyesha jitihada za makusudi katika kutetea maslahi ya wakulima yanayotokana na kilimo chao.

Anafafanua kuwa ugonjwa huo ulianza kwa kushambulia migomba ya wakulima katika vijiji vya Rubagano, Kigaga, Ggwampala, Kabaya, Chomma na Kabatagi vyote vikiwa katika kata ya Mwizi wilayani Mbarara na kusababisha hali ya uchumi wa wakulima kudorora ingawa kwa sasa hali imekuwa tofauti kwa wakulima hao kwani wameweza kushirikiana kuutokomeza.

Kama walivyofanya wakulima wa Uganda, wakulima wa Bukoba hawana budi kushirikiana kuhakikisha ugonjwa huo unatokomezwa.



MIGOMBA ikiwa imeathirika kwa ugonjwa.



MIKUNGU ya ndizi kama hii inaweza kupungua ubora kutokana na ugonjwa wa migomba.